**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR NAM. 1 YA 2012 NA KUTUNGA UPYA SHERIA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nianze Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, ambae ameumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake na kuviwekea taratibu ili zifuatwe. Pia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha leo hii kutekeleza majukumu yetu kwa amani na usalama wa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Nam. 1 ya 2012 na Kutunga Upya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekma na busara pamoja na afya njema itakayokuwezesha kutekeleza vyema majukumu yako na kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa, Mwl. Haroun Ali Suleiman kwa mashirikiano yake aliyoipatia Kamati hii wakati wa kuupitia Mswada huu lakini pia, nje ya Mswada huu amekuwa nasi bega kwa bega wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ili aweze kutusaidia zaidi katika kujenga mustakbali bora wa Nchi yetu kwenye masuala ya kukuza Utawala Bora. Kamati pia inamshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt Mwinyi Talib Haji kwa msaada wake na ushirikiano wake katika majadala wakati Kamati ilipokutana na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, napenda kuwashukuru watendaji wake wote katika Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Ndg. Mansura M. Kassim kwa kusimamia vyema na kuandika upya Sheria hii ambayo inakwenda kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka na kusimamia vyema mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; kazi ambayo imefanywa vyema sambamba na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hii katika kuifanya iwe bora kwa misingi ya utawala wa haki na utawala bora.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa niwashukuru wadau wote wa Mswada huu ambao wameipitia kwa nafasi zao lakini pia wadau ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ya kujenga na kuiwezesha Kamati kupata upeo mpana zaidi katika Masuala ya Rushwa na Uhujumu Uchumi hapa Zanzibar na Tanzania kwa Ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, pongezi za pekee ziende kwa wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa juhudi zao walizozionyesha katika kuwapatia wajumbe wa Kamati hii maarifa kuhusu mswada huu na kuwaelekeza mambo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuufanya Mswada huu uwe bora na wenye kuendana na wakati huu wa mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, sambamba na kuifanya Zanzibar kuweza kupambana na makosa hayo.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kutekeleza wajibu wao kikanuni kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 84 (5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati kutokana na ubora wa mswada wenyewe. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa ili kujisomea kwa ufafanuzi na ufahamu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa madhumuni ya Mswada huu pamoja na mambo mengine ni Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Nam. 1/2012 na kutunga upya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, ambayo inaelezea uanzishwaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Mamlaka na kusimamia vyema mapambano dhidi ya makosa ya Rushwa na uhujumu Uchumi. Kamati inashauri Kifungu cha 3 cha Mswada huu kuweka maana nzuri yenye kueleweka bila kuwa na utata ndani yake, kifungu hiki kurekebishwa katika tafsiri ya neno **"Wakala",** aya ya (a) kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

> **"mtu aliyeajiriwa ikiwa yupo katika mkataba wa ajira, mkataba wa huduma au vyenginevyo ,ajira ya kudumu au ya muda au kwa malipo au bilaya malipo".**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, inashauri katika Kifungu cha 12 vifungu vidogo vya Sheria hii vinarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kifungu kidogo cha (1) kinafutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

   **"Mamlaka inaweza kuanzisha idara, vitengo, divisheni, sehemu au ofisi nyengine kama itavyoonekana inafaa kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake".**

b) kifungu kidogo cha (2) kinarekebishwa kwa kuingizwa maneno **"wa Mamlaka"** baina ya neno "**Makamanda"** na **"wa**" ili kuleta maana sahihi kwa watumiaji wa sheria hii.

c) Kufutwa maneno **"kwa kushauriana na mkuu husika"** yaliopo mwishoni mwa kifungu kidogo hicho ambapo maneno hayo maana yake imeshajirudia katika kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya tano ya Mswada huu inayohusu makosa ya Rushwa katika Kifungu cha 40, Kamati inashauri Kuongeza kifungu kidogo cha 2 ambacho kitaelezea maana halisi ya **"Afisa wa Mahakama"** na kitasomeka kama ifuatavyo:

> **"Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "Afisa wa Mahakama" maana yake ni Jaji, Hakimu au muajiriwa mwengine yeyote wa Mahakama au mtu mwengine yeyote mwenye ushawishi katika maamuzi ya Mahakama".**

**Mheshimiwa Spika,** katika Kifungu cha 75 kinachozungumzia *Amri ya kuzuia mali inayotuhumiwa*, Kamati inarekebisha kifungu kidogo cha (2) kwa kufutwa na kuandikwa upya kutokana na kuonekana makosa mengi ya kisarufi ambayo kama hayatofanyiwa marekebisho yanaweza yasilete maana iliyokusudiwa ndani ya kifungu hicho, marekebisho yenyewe ni kama ifuatavyo:

> **"(2) Endapo mtuhumiwa atakuwa chini ya uchunguzi kutokana na kosa la rushwa au uhujumu uchumi, kwa ombi la Mkurugenzi Mkuu, Mahakama kwa kuzingatia masharti na muda ulioombwa au vyenginevyo kama itakavyoona inafaa, inaweza kutoa amri ya:**
>
> **(a) uzuiaji wa fedha zote zinazomilikiwa na mtu aliyetajwa katika amri hiyo na mali nyengine zinazodaiwa au zinazomilikiwa na au kwa niaba ya mtuhumiwa; na**
>
> **(b) kumkataza mtuhumiwa au mtu mwengine yeyote anayefanya kazi kwa niaba yake au mtu mwengine yeyote aliyetajwa katika amri, kuhaulisha, kuweka rehani au kuuza katika njia yoyote pesa au mali iliyozuiliwa".**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na yote, Kamati imependekeza kufanyiwa marekebisho madogo katika kifungu cha 90 cha Mswada, kwa kuondolewa kifungu hicho kinachohusu Ripoti za mwaka katika Sehemu ya Kumi ya Masharti ya Fedha na kuwekwa badala yake Sehemu ya Kumi na Moja ya Masharti Mengineyo. Hii ni kutokana ripoti zilizotajwa hapa zinahusiana na ripoti za utekelezaji wa ZAECA ambapo kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi haitaathiri utekelezaji wake na

kitasomeka kama ifuatavyo:

**(1) Mamlaka itaandaa ripoti ya Mwaka na itaiwasilisha kwa Rais ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka husika.**

**(2) Ripoti ya mwaka itajumuisha maelezo kuhusu kazi zilizofanywa na Mamlaka.**

**(3) Rais, baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atamuidhinisha Waziri kuiwasilisha ripoti hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi.**

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na yote, imependekeza kurekebishwa kwa Kifungu cha 93 kifungu kidogo cha (5) kinachozungumzia *ushughulikiaji wa mali iliyotelekezwa* kwa kufutwa na kuandikwa upya ili kuweka urahisi wa utekelezaji wa kifungu hicho kama ifuatavyo:

**"Endapo Mahakama inaona kwamba mali iliotelekezwa inaweza kuoza kwa haraka au inahitaji kuuzwa kwa manufaa ya mmiliki, itaizuia au kutoa amri ya kuzuia na inaweza wakati wowote kuelekeza kwamba iuzwe au iharibiwe bila ya kutoa notisi na baada ya mauzo au uharibifu huo, Mahakama itatoa amri ya notisi ya mauzo au uharibifu huo itolewe kwa utaratibu uliolezwa chini ya kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hiki".**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, Kamati baada ya kutafakari kwa makini imeona umuhimu wa Mamlaka hiyo, hivyo basi inashauri Serikali kuwapa nguvu ya kutekeleza majukumu yake kwa kuweka utaratibu maalumu wa kuupatia vitendea kazi na fedha za kutosha ili waweze kuwajibika vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kuhitimisha hotuba hii kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu ya kwamba waungane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati imepata muda wa kutosha wa kuupitia na kuuchambua kifungu kwa kifungu kwa mashirikiano na wataalamu wetu wa sheria ili kuufanya uwe bora na wenye kuleta maslahi kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaenda kuwa kipengele muhimu cha kukuza na kulinda uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha**.

Ahsante,

……………………………

(*Machano Othman Said*)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR